Wema Na Kweli

na

Terry Warford

Wema Na Kweli

na

Terry Warford

Novemba 5, 2011

Wema Na Kweli

Wiki hii nilisoma kitabu ambacho kilinikatisha tama sana. Kilikuwa ni kitabu cha watoto ambacho binti yangu alitoka nacho maktaba. Muundo ulikuwa nzuri; tendo lilikuwa zuri. Kilichonikatisha tamaa ni maudhui ya kitabu.

Maudhui, au ujumbe, wa kitabu ulikuwa kwamba wakati mwingine unapaswa kusema mambo ambayo sio mazuri kiukweli, au kusema vitu ambavyo sio vya kweli ili uwe mwema. Swala lililetwa kuhusu kijana mdogo aliyekuwa mwanagenzi kwa bibi kizee, akawa amezeeka na kuwa wa kijivu. Waka wa mwisho wa huduma, mama huyu alimuuliza kijana kama alikuwa anaonekana mbaya. Kwa wema, asingeweza kusema kwamba bibi huyu alikuwa na muonekano mbaya, na hivyo akaanguka jaribio la kweli. Kweli ililetwa kama kweli iwe kweli, bila kujali kuhusu wema au kutokuwa mwema, au mzuri au muovu. Watu wengi katika ulimwengu huu wanatumia fikira kama hii: wakitumia uaminifu kama udhuru wa kuwa katili, au wema kama udhuru wa kusema uongo.

Vyema, ndugu na dada, Bwana amenibariki kwa kuleta mengi kuhusu watu wa zamani katika maisha yangu. Na ninapofikiria kuhusu upendo na kujali kwao, upole wao kwangu, na uimara katika maandiko, huwezi kunishawishi kwamba walikuwa wabaya, hata kama walikuwa wamezeeka na kijivu.

Natumai katika makala hii, kwa msaada wa Mungu, kuangamiza (au ikinge) mawazo yako kwamba uaminifu unaweza kuwa kutokuwa mwema au mwema siyo kweli.

Kwanza kabla ya yote, wema na kweli yanakwenda bega kwa bega kwa sababu vyote vimetoka kwa Mungu.

Katika Yohana 17:17, Yesu alipokuwa anamuomba Mungu, Alisema, "*Uwatakase na hiyo kweli: neno lako ndiyo kweli.*" Pia tunaona katika 1 Yohana 4:8 kwamba Mungu ni pendo, "*Yeye asiyejua kupenda hakumjua Mungu; maana Mungu ni pendo.*" Vyote vilitoka kwa Mungu. Lazima zifanye kazi pamoja.

Fafanuzi ya upendo inajumuisha wema na kweli. 1 Kor. 13:4-6, "*Upendo huvumilia, hufadhil, upendo hausudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli;*"

Angalia ni mara ngapi huruma na kweli vinaunganishwa katika maandiko. Mith. 3:3, "*Rehema na kweli zisifarakane nawe; zifunge shingoni mwako; ziandike juu ya kibao cha moyo wako*". Huruma na

neema bila shaka vyote ni wema, na vinaunganishwa katika kweli ndani ya maandiko.

Kwa upande mwingine, uongo hautokani na wema. Biblia inatuambia kwamba kinyume cha uongo ni kuchukia. Mith. 26:28, "*Ulimi unenao uongo huwachukia wale uliowajeruhi; na kinywa cha kujipendekeza hutenda uharibifu.*"

Hatuwezi kutumia wema kama udhuru wa kusema uongo.

Au kutumia huruma kama udhuru wa kuwa wajinga. Kabla hatujaita majina ya watu, tunapaswa kukumbuka kwamba Mungu alimfanya mtu huyo kwa mfano wake. Yak. 3:8-10, "*Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga; ni uovu usiotulia, imejaa sumu iletayo mauti. Kwa hiyo twamhimidi Mungu Baba yetu, na kwa huo twawalaani wanadamu waliofanywa kwa mfano wa Mungu. Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana, ndugu zangu haifai mambo hayo kuwa hivyo.*" Kama tunamuita mtu "mbaya" au "pumbavu" au majina mengine ya kijinga, nisawa kwamba tunamuita Mungu katika maneno haya, kwa sababu tumeumbwa kwa mfano wake. Je! Kwa uaminifu tunaweza kumpa Mungu majina? Hapana. Hivyo hatuwezi kwa ukweli kuwaita watu wengine majina, pia.

Sababu ya kuwa wajinga kwa watu wengine inajulikana kama uchafu, siyo huruma. Na uchafu ni kitu ambacho tunapaswa kuweka mbali katika maisha yetu. Efe. 4: 31-32, "*Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*"

Mara nyingi watu huropoka kitu cha kwanza kinacho kuja katika akili zao, hata kama ni kibaya, na kuiita huruma, au kuongea akili zao. Katika ukweli ni kuwa haraka na ndimi zetu. Mith. 29:20, "*Je umemuona mtu mwenye kuhamaki katika maneno? Afadhali kumtumaini upumbavu kuliko yeye.*" Kufikiri kupitia maneno yetu sio kutokuwa na huruma. Ni haki na ndio tumeamriwa kufanya. Mith. 15:28, "*Moyo wa mwenye haki hufikiri jinsi atakavyojibu; bali kinywa cha wasio haki humwaga mabaya.*"

Ndiyo, maranyingi kuna ukweli usiopendeza kuweza kunenwa, hata kukemea na kuadibisha. Bado haya yote yanapaswa kushughulikiwa katika wema iwezekanavyo, tukiyafikiria, na kuyatoa kwa ajili ya faida ya watu wengine.

2 Tim. 4:2, "*Lihubiri neno uwe tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.*" Hata kama ukweli haupendezi, maneno yetu lazima yawe na neema.

Hivyo, natumaini tumethibitisha kipengele chetu: kwamba tusitumie huruma kama udhuru wa kuwa wajinga, au wema kama udhuru wa kusema uongo. Huruma na kweli utenda kazi pamoja kama tukiishi maisha yetu katika njia ya Mungu.

Hebu tufunge na maneno ya Yesu katika Math. 7:12, mara nyingi inachukiliwa kama muongozo dhabiti: “”.

Katika jina la Yesu,

Ndg. Terry Warford